JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO

**SHULE YA SEKONDARI MKUU**

Simu: 0764613031– Mkuu wa Shule.
0767244926 / 0759399939 – M/Mkuu wa shule.
Blog: www.mkuutaaluma.blogspot.com
Email: hos.mkuu@gmail.com
mkuutaaluma@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI MKUU,
S.L.P 145,
**MKUU – ROMBO.**

Tarehe: **30/05/2021.**

Mzazi/Mlezi/Mfadhili wa Mwanafunzi:……………………………………………………………

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MKUU MWAKA 2021/2022**

**A. UTANGULIZI:**

Kwa niaba ya Jumuiya ya Shule ya Sekondari Mkuu iliyoko Wilaya ya Rombo Mkoa wa Kilimanjaro, ninayo furaha kukujulisha kwamba mwanao…………………………………… aliyekuwa akisoma shule ya Sekondari ………………………………… amechaguliwa kujiunga katika Shule ya Sekondari Mkuu kidato cha Tano kwa mwaka huu wa **2021/2022**. Shule itafunguliwa tarehe **…..../07/2021** na mwanao afike tarehe hiyo shuleni ili aweze kusajiliwa.

Shule ya Sekondari Mkuu ni shule nzuri ambayo ni mchanganyiko wa wanafunzi kuanzia Kidato cha I – VI. Wanafunzi wasichana wa kidato cha tano na sita wanakaa kwenye mabweni yaliyopo shuleni. Shule ya Sekondari Mkuu iko katika mazingira mazuri ya mwanafunzi kusoma na kuweza kufaulu vizuri kama ataonyesha bidii ya kusoma. Shule inao walimu wa kutosha na huduma zote muhimu kwa wanafunzi zinapatikana shuleni. Mwanao aitumie nafasi hiialiyopewa na Serikali ili baadaye alisaidie Taifa letu, wazazi wake na yeye mwenyewe.
Tunakupongeza wewe mzazi pamoja na mwanao kwa kupata nafasi hii.

**B. USAFIRI WA KUFIKA SHULENI**

Mwanafunzi akifika Moshi mjini kituo kikuu cha mabasi akitokea popote pale, aulize na kupakia magari yaendayo Rombo kupitia Mwika hadi Tarakea. Shule yetu ipo umbali wa kilomita 60 kutoka Moshi mjini hadi Mkuu Rombo kabla hujafika Tarakea. Nauli ya kutoka Moshi mjini hadi Mkuu Rombo ni Tshs. 3000 hadi Tshs. 4000 kutegemea na gari. Kwa wanafunzi wanaotoka Dar es Salaam au kupitia Dar es Salaam wapande magari ya *Dar express*, *Tilisho*, *Esther luxury,* yanayokuja moja kwa moja Rombo. Kwa wanaotoka Dodoma wapande *Shabiby, Extra coach* na wanaotoka Singida wapande *Mtei express.* Kwa wanaotoka Mwanza na maeneo mengine ya kanda ya ziwa wapande mabasi yanayofika hadi moshi mjini na kisha kupanda usafiri mwingine hadi shuleni.

**C. KITUO CHA KUTEREMKIA**

Ukitokea Moshi mjini mwambie kondakta wa gari utateremkia ***Mkuu Kanisani*** vilevile kwa wale wanaotokea Tarakea kuelekea Moshi nao watateremkia ***Mkuu kanisani***. Kutoka hapo Mkuu Kanisani kuelekea shuleni ni umbali wa mita 150 utakuwa umefika shuleni. Ukifika shuleni utaripoti na kupokelewa na mwalimu wa zamu au Makamu wa Mkuu wa shule ambao wote watakuwepo shuleni kwa kipindi hicho. Baada ya kuripoti shuleni utasajiliwa ofisini kwa Makamu wa Mkuu wa shule ukiwa na mahitaji yote muhimu uliyoagizwa kuleta shuleni.

**D. HUDUMA ZINAZOPATIKANA SHULENI:**
Shule inalo duka ambalo hutoa huduma za mahitaji karibu yote muhimu kwa wanafunzi na watumishi wote wa shule. Zahanati ya Mission Mkuu iko karibu na shule. Hospitali kubwa ya Wilaya ipo karibu na shule, usafiri wa kuja shuleni na kurudi nyumbani ni mzuri kwani shule ipo karibu sana na barabara, Benki, Posta vyote viko karibu.

**E.** ***Wanafunzi wasio na bima ya afya wanashauriwa kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya NHIF ambayo kwa wale watakao hitaji watachangia sh 55,000/= kwa mwaka na waje na fedha hiyo wataelekezwa utaratibu wa kujiunga. Aidha gharama za matibabu kwa mwanafunzi litakuwa ni jukumu la mzazi kwa kipindi chote atakachokuwa shuleni kama hatakuwa na bima*.**

**F. MAHITAJI YA KULETA SHULENI MWANAFUNZI:**

**1) SARE YA SHULE:**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na sare ya shule iliyoshonwa vizuri kwa maadili ya mwanafunzi awapo shuleni. **Nguo za kubana na fupi marufuku na mwanafunzi hatapokelewa**.

**WASICHANA**
- Sketi mbili (02) rangi **nyeusi cotton** inayozidi magoti kwa urefu unaokaribia kwenye viatu mshono – "**Rinder box**" **mbele na nyuma pembeni marinda madogo**.
- Shati mbili (2) nyeupe mikono mirefu.
- Waje na neck tai nyeusi.
- Soksi nyeupe ndefu jozi 2 au zaidi, Na viatu vyeusi vya kamba jozi mbili au zaidi.
- Nguo za michezo pair moja truck suit rangi ya dark blue yenye kofia (Apple), pamoja na raba pair moja.
- Nguo za kazi shamba dress utashona Shuleni kwa gharama ya Tsh; 15,000/=
- Mwanafunzi aje na tranka ya chuma kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake na begi la daftari tu.
- **Mwanafunzi aje na tochi/ taa ya solar na mwamvuli kwa ajili ya kujikinga na mvua**

**N.B:**
- Kwa wasichana Waislamu wanaruhusiwa kuvaa HIJABU Nyeupe ya sketi.
- Mwanafunzi aje na **Sweta ya Shule Nzito Rangi Nyeusi** yenye kola ya "**V**.(Inashauriwa mtoto kuwa na sweta mbili)
- **Mzazi anashauriwa kununua T-shirt nzito rangi ya Dark Blue (form six) kwa wale watakaoshindwa kuipata itapatikana shuleni yenye nembo kwa gharama ya Tsh; 12,000**
- Kwa sababu ya hali ya baridi mzazi unashauriwa kumshonea mwanao suruali mbili rangi ya kijani kibichi ya kuvalia na shamba dress. Pamoja na pull neck ya rangi nyeusi.

***N.B; Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo nyingine tofauti na sare tajwa.***

**2) ADA NA MICHANGO MINGINE YA SHULE:**

**a. ADA** ya shule kwa mwaka ni shilingi **70,000** (*Shilingi **35,000/=** kwa muhula mmoja*).

**b. MICHANGO MINGINE YA SHULE NI KAMA IFUATAVYO;-**
- Ukarabati wa (viti,meza,mabweni na gari) …………….. 15,000/=
- Kitambulisho na picha ………………………………… . 6,000/=
- Taaluma ………………………………………………… 20,000/=
  Walinzi ,Wapishi na Vibarua wengine ………………… 30,000/=
- Mchango wa mahafali ………………………………….. 20,000 /=
- Nembo ya shule ……………………………………….. . 2,000/=
- Mtihani wa kujipima ……………………………..  20,000/=
- Tahadhari (Haitarejeshwa) …………………………… . 5,000/=

**Jumla ya michango yote shuleni ……………………** Tsh **188,000/=**

Ada na michango mingine iliyotajwa hapo juu ilipwe kwenye akaunti ya shule

**MKUU SEC. SCHOOL A/C No: 40406600024 NMB .**

- ***Godoro la kulalia lina patikana shuleni kwa kiasi cha Tsh; 20,000 kwa mwaka lipa kwenye akaunti namba 40410021226 (MIRADI MKUU SEKONDARI NMB)***
- ***Mchango wa bweni Tsh 100,000. Lipa fedha hiyo kwa akaunti namba 40410021226 (NMB) MIRADI MKUU SEKONDARI***

**NB:** ***Hatupokei fedha taslimu malipo yote yafanywe kupitia benki.*** Unaweza kulipia michango hiyo popote kwenye tawi la NMB. Baada ya kufanya malipo hayo Mwanafunzi au mzazi anatakiwa kuleta "**Bank Pay In Slip** shuleni siku ya kuripoti ili aweze kukatiwa stakabadhi ya Serikali kwa malipo aliyoyafanya na kusajiliwa.

**G. MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA KUJA NAYO SHULENI KWA WOTE**

- Ream 1 ya karatasi nyeupe A4.
- Ream 1 Ruled Paper (yenye mistari)
- Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
- ***Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia (Mwanafunzi anayesoma anapaswa kununua) itakaguliwa wakati akifika shuleni.***
- ***Scientific calculator (Mwanafunzi anapaswa kuja nayo)***
- Shuka mbili rangi ya Pink, Blanketi moja, mto na foronya
- Vyombo vya chakula: Sahani, Bakuli, Kijiko na Kikombe *(Vinauzwa duka la shule kwa wale wasiokuja navyo)*
- Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko na kandambili za kuogea (Atanunua akiwa shuleni kwa anayehitaji)

**Vifaa vya usafi**

CBG – Kwanja 1, squizer 1
PCB – Soft broom 1, Jembe 1
PCM – Fagio ya chelewa 1, squizer 1
HGE – Ndoo 2 kubwa, Hard bloom 1 (Za kusugulia sakafu)
HGL -
HKL - } Ndoo mopu ya plastiki moja (Inayotumika wakati wa kudekia)
HGK -

**N.B** .Kwa wale wanaotoka mbali vifaa vinapatikana maeneo karibu na shule.

**H. MAHITAJI YA DARASANI**

Madaftari makubwa ya kutosha, kalamu, rula, penseli, mathematical set, Scientific calculator, file kwa kila somo (kwa masomo ya msingi- principle subjects) kwa ajili ya kutunza mitihani na majaribio n.k .

**I. FOMU MBALIMBALI KWA MZAZI NA MWANAFUNZI ZA KUJAZA:**

Fomu mbalimbali za kujazwa kwa mzazi na mwanafunzi zimeambatanishwa.

**J. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE ZIMEAMBATANISHWA:**

- ***Mwanao azisome vizuri na kuzielewa na awe tayari kufuata maelekezo na taratibu nyingine za shule.***

Mwisho tunamtakia mwanao safari njema ya kuja hapa Shule ya Sekondari Mkuu.

**Asante.**

**………………**

K. MASHIMBA

MKUU WA SHULE

NB: ***Mzazi/mlezi tunaomba uthibitishe mwanao kujiunga na shule yetu mara tu upatapo nafasi ya uchaguzi wa serikali wakati ukiendelea na maandalizi mengine kwa namb 0764613031/ 0754601392 (Mkuu wa shule) au 0759399939 (Makamu mkuu wa shule). Changamoto yeyote itakayojitokeza wasiliana na uongozi wa shule***

## (KIAMBATANISHO Na. 1)

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
## SHERIA ZA SEKONDARI……………………..………. (TANZANIA)

### 1. HESHIMA NA UTII

i. Ni lazima kila mwanafunzi atii viongozi wote kuanzia walimu, wafanyakazi, viranja na wale wote waliomzidi umri.

ii. Ni lazima kila mwanafunzi asimame na kusalimu viongozi na wakuu wote na wote waliomzidi umri.

iii. Ni lazima kila mwanafunzi aitike mara moja na kukimbilia mahali anapoitwa wakati asikiapo kengele au wito mwingine wowote.

iv. Ni lazima kila mwanafunzi atii maagizo kwanza kabla ya kujenga hoja.

### 2. MAHUDHURIO NA KUWAHI

i. Ni lazima kila mwanafunzi awepo shuleni muda wote anaotakiwa.

ii. Ni lazima kila mwanafunzi ahudhurie na kushiriki katika vipindi vyote ndani na nje ya darasa.

iii. Iwapo mwanafunzi ameshauriwa kutofanya kazi Fulani kwa sababu za kiafya, UTHIBITISHO wa Daktari wa Hospitali ya Serikali utahikajika.

iv. **Mwanafunzi akikosa shule kwa zaidi ya siku tatu (3) mfululizo muhula mmoja bila sababu zenye kukubalika na shule atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo**.

### 3. UVAAJI WA SARE ZA SHULE

i. Ni lazima kila mwanafunzi awe msafi wa mwili na mavazi.

ii. Sare ya shule ni lazima ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo shuleni na wakati wowote atakapohitajika kuvaa akiwa nje ya shule.

iii. Mashati na blauzi ni lazima yachomekewe, vishikizo vyote viwepo na kufungwa. Nywele ziwe fupi na zilizochanwa na nadhifu

N.B; ***Ukiukwaji wa uvaaji wa sare za shule utasababisha mwanafunzi apewe adhabu kali ikiwa ni pamoja na kurudishwa nyumbani***

### 4. MWANAFUNZI HARUHUSIWI:

**i.** Kuwa na kucha ndefu

**ii.** Kupaka nywele au macho au mdomo rangi

**iii.** Kukaanga nywele (kuweka nywele dawa).

**iv.** Kuvaa kilemba, kofia, hereni, mkufu, vipuli, pete na mapambomengine mbalimbali.

**v.** Mwanafunzi haruhusiwi kutumia simu ya mtu yeyote isipokuwa itakayoelekezwa na uongozi wa shule vinginevyo akibainika hatua za kinidhamu zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kurudishwa nyumbani

**vi.** Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima kama vile mini sketi, kaputla

**vii.** Kunyoa kipara, panki au kiduku

**viii.** Kufuga nywele ndefu au kusuka

**ix.** Kuwa na begi la nguo.

### 5. LUGHA YA MAWASILIANO

i. Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza tu isipokuwa kwenye somo la Kiswahili na dini ikibidi. Wanafunzi watawasiliana na watu wengine kwa lugha ya Kiswahili ikibidi.

ii. NI MARUFUKU kwa mwanafunzi kuwasiliana kwa lugha nyingine yoyote.

iii. Lugha chafu ya matusi HAIRUHUSIWI shuleni.

### 6. USAFI WA MAZINGIRA

i. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuweka eneo la shule na majengo ya shule katika hali safi.

ii. Vyoo na ukumbi wa chakula ni lazima viwe safi na vitumiwe ipasavyo.

iii. Uchafu/takataka ni lazima zitupwe jalalani.

## 7. KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE

NI MARUFUKU kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo au kazi nyingine nje ya darasa bila ruhusa. Ruhusa itatolewa na mwalimu wa zamu na kuidhinishwa na Mkuu wa shule au makamu mkuu wa shule na kupewa kibali maalumu (*permission slip*) na mara arudipo akirudishe kibali kwa mwalimu wa zamu.

Mwanafunzi awapo shuleni NI MARUFUKU kutembea sehemu zifuatazo bila sababu maalumu:

i. Chumba cha walimu (Staff-Room)
ii. Nyumba za walimu na watumishi wasio walimu.
iii. Ofisi na Stoo za shule.
iv. Jikoni.
v. Karakana na maabara.
vi. Sehemu zenye mashamba na mifugo.

## 8. MICHEZO

Ni lazima kila mwanafunzi ashiriki katika michezo inayofanyika shuleni. Hivyo awe na nguo za michezo kama viatu(raba), T-Shirt au "Truck Suit". Kwa wale wenye changamoto za kiafya waje na maelezo ya daktari.

## 9. ADHABU ZINAZOTOLEWA NA SHULE

i. Kuonywa kwa mdomo wa maandishi
ii. Kurudishwa nyumbani kwa muda ama kufukuzwa shule.
iii. Kufanya kazi za nje.
iv. Kufikishwa katika kamati ya nidhamu kwa hatua kali za kinidhamu.
v. Kuchapwa viboko.

## 10. MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Ulevi wa pombe au madawa ya kulevya
iii. Uvutaji bangi/sigara
iv. Kuanzisha au kushiriki katika mgomo au fujo za aina yoyote shuleni
v. Kutoheshimu alama za Taifa kama vile Bendera ya Taifa, picha ya Rais ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Makamu wake, Fedha ya Tanzania n.k
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
vii. Uasherati
viii. Kupata mimba au kutoa mimba
ix. kuolewa
x. Kukataa adhabu iliyotolewa na uongozi wa shule
xi. Kupigana au kumshambulia mtu yeyote au kuzomea au lugha ya matusi
xii. Kutohudhuria masomo
xiii. Utoro wa vipindi wa muda mrefu
xiv. Kukataa kufanya mazoezi ya mitihani
xv. Kukataa kufanya usafi wa maeneo shuleni
xvi. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi
xvii. Mwanafunzi kuwa na radio shuleni. Vyombo vya habari vipo shuleni eg. TV.
xviii. Kuja na pasi shuleni.
xix. Kuwa na manukato (spray, perfume na lotion zenye harufu kali)
xx. Kuchubua Ngozi.

N.B; ***Mzazi/mlezi utalazimika kufika shuleni pindi mwanao abainikapo kuwa na makosa hayo na utaondoka naye kwenda nyumbani***

**(KIAMBATANISHO Na. 2)**

## KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

### WAJIBU WA MWANAFUNZI ANAYESOMA SEKONDARI

Mwanafunzi yeyote anatakiwa afahamu, azingatie na afuate taratibu zifuatazo:

1) Kuwa na heshima kwa walimu, Watumishi wengine na wote waliomzidi umri na wadogo.
2) Kuongea lugha safi isiyo na matusi wala kashfa kwa binadamu yeyote awaye.
3) Kushiriki na kusaidiana katika kazi za shule.
4) Kuwahi shule, kufanya kazi zote za shule kuendana na maagizo yatolewayo na uongozi wa shule.
5) Kuhakikisha kwamba mazingira ya shule anakoishi yanakuwa safi wakati wote, kwa kufanyia usafi.
6) Kusimama na kusalimia wakubwa wanapopita mbele yake na walimu wanapoingia darasani.
7) Kupokea kwa heshima mizigo kwa watumishi wa shule na wageni wa shule na kuwasaidia.
8) Kuheshimu bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, wimbo wa Shule, Nembo za Taifa, Fedha za Taifa, Picha za viongozi wa serikali, n.k.
9) Kutii na kuheshimu wito wowote unaotolewa shuleni na kengele inapopigwa.
10) Kutii na kuheshimu wito na kengele mara tu inapogongwa.
11) Kuheshimu mahali pa mikusanyiko kwa utulivu, na kufuata utaratibu uliowekwa.
12) Kuheshimu na kutunza Mali za Umma na binafsi.
13) Kusoma kwa bidii, na kufanya mazoezi ya mitihani yote inayotolewa na Taifa.
14) Kulipa ada na michango mingine ya shule bila kuchelewa.
15) Kufuata sheria zote za shule.
16) Kuwa mzalendo kwa mambo yote yanayohusu shule, Jamii na Taifa

**-*(KIAMBATANISHO Na. 3)**

## MKATABA NA KAULI YA KUKUBALI KUTII SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Mimi…………………………………………………………………(*Jina la mwanafunzi*)
Ninakiri kuwa nimesoma na kuzielewa vizuri sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyoainishwa katika vipengele vyote, na kuwa mara nikiukapo sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe kama zilivyoainishwa dhidi yangu.

JINA LA MWANAFUNZI………………………………………………..

SAHIHI YA MWANAFUNZI……………………………………………..

TAREHE…………………………………………………………………….

Mimi ……………………………………………………….(*Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi*) wa mwanafunzi……………….……………..(*Jina la mwanafunzi*) wa kidato cha………………

tahasusi(*comb.)* ya………………..

Nakiri kupokea, kusoma na kuzielewa taratibu zote zilizo kwenye maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari ya Mkuu. Iwapo mwanangu atakiuka taratibu hizo nitakuwa tayari kukubali hatua zitakazochukuliwa dhidi yake na shule. Nitakamilisha mahitaji yote ya shule kwa wakati.

JINA LA MZAZI/MLEZI ………………………………………..…………

Namba za simu……………………………………………………………

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI………………….………………………….

TAREHE………………………………………..

Namba ya simu ya ndugu/Jamaa wa karibu………………………………….

**(KIAMBATANISHO Na. 4)**

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
**MKUU SECONDARY SCHOOL**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a medical Officer in a Government hospital in respect of all new students to Mkuu Secondary School.

STUDENT'S FULL NAME: ……………………………………………………………………….

AGE: ………………………………………………………..

1. Blood count (Red and White): ………………………………………………
2. Stool Examination: ……………………………………………………………………
3. Urine Examination: ……………………………………………………………….
4. Eye test: ……………………………………………………………………
5. Ear test: …………………………………………
6. Speech test: ……………………………………………………………………
7. T.B test: ………………………………………………………………………………
8. STD test: ………………………………………………………………………………
9. Spleen: ………………………………………………………………………………………
10. Abdomen: ……………………………………………………………………………………..
11. Additional information from any Physical, Mental, Hereditary diseases or disabilities:

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

*Treatment after Examination*:

………………………………………………………………………………………………………

MEDICAL CERTIFICATE

*I certify that the above-mentioned student has been thoroughly examined by me and found fit/unfit to pursue further education.*

*SIGNATURE*: ……………………………………………………………………………….

*DESIGNATION/STAMP*……………………………………………………………….

*DATE*: ………………………………………………………………..

*STATION*: ……………………………………………………………